JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# WIZARA YA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI

**TAMKO LA MHESHIMIWA JERRY WILLIAM SILAA (MB), WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA KATIKA MAADHIMISHO YA 45 YA SIKU YA UMOJA WA POSTA AFRIKA TAREHE 18 JANUARI, 2025**



*Mhe. Jerry W. Silaa (MB)*

*Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari*

**Kauli Mbiu: "Posta: Sekta Jumuishi kwa Maendeleo Endelevu ya Kijamii."**

Ni heshima kubwa kwangu kuungana na Mawaziri wenzangu wanaosimamia Sekta ya Posta kutoka nchi za Afrika katika kuadhimisha miaka 45 tangu kuanzishwa kwa Umoja wa Posta Afrika, ni tukio muhimu katika historia ya bara letu. Leo, tunasherehekea si tu mafanikio tuliyopata, bali pia uwezo na ubunifu katika kukuza na kuendeleza Sekta. Tunakumbuka kuanzishwa kwa Umoja huu, tunasherehekea mafanikio tuliyonayo na kuthibitisha dhamira ya dhati inayolenga kuwa na Sekta jumuishi katika maendeleo kote Afrika.

Kauli Mbiu ya mwaka huu inasema: "**Posta: Sekta Jumuishi kwa Maendeleo Endelevu''.** Kauli Mbiu hii inaendana na lengo kuu la Umoja wa Posta Afrika ambalo limejielekeza kusaidia Mashirika ya Posta Afrika si kutoa huduma ya kusafirisha barua na vifurushi pekee, bali pia kutoa fursa, kukuza uchumi, na kuimarisha mshikamano miongoni mwa jamii. Ninashukuru kwamba Umoja wa Posta Afrika (PAPU) unaendelea kushirikiana na Serikali kuleta maendeleo katika nchi zetu za Afrika.

Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari inaunga mkono Kauli Mbiu ya mwaka huu kwa kuwa Wizara imelenga kuhakikisha Sekta ya Mawasiliano, hususan Sekta ya Posta, inaendelea kutoa huduma bora na za kuaminika za posta na usafirishaji wa haraka. Kwa kuwa ni Wizara inayojihusisha na maendeleo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, tutaimarisha ujenzi wa miundombinu ya TEHAMA na programu za uhamasishaji kote nchini ili wadau wote katika Sekta ya Posta na Sekta nyingine watumie TEHAMA katika kubuni na kuanzisha bidhaa mpya pamoja na utoaji wa huduma.

Wakati tunasherehekea maadhimisho ya miaka 45 ya Siku ya Posta Afrika, lazima pia tuangalie changamoto zinazotukabili na kuzigeuza kuwa fursa za kujenga Sekta imara zaidi. Sekta ya Posta, ambayo hapo awali ilionekana hasa kama njia ya kusafirisha barua na vifurushi pekee, imekuwa kiungo muhimu katika ukuaji kijamii na kiuchumi. Imekuwa kiunganishi kwa mamilioni ya watu, hasa katika maeneo ya vijijini na yasiyo na mvuto kibiashara ambapo upatikanaji wa huduma kwa jamii uko kwa kiwango cha chini. Huduma za posta ni zaidi ya utumaji wa barua; imekuwa kiunganishi muhimu katika mawasiliano na biashara na kusaidia usafirishaji wa kuaminika wa vifurushi na bidhaa mbalimbali.

Nchi za Afrika na dunia kwa ujumla zinabadilika kwa kasi kutokana na matumizi ya kidijitali, hivyo Sekta ya Posta lazima iendane na kasi hiyo kwa kuanzisha majukwaa ya kidijitali yanayowezesha biashara mtandao, kuwa na huduma za fedha kidijitali, na mawasiliano ya kielektroniki. Ni lazima kama Sekta, tukubali kuendana na mabadiliko ya kidijitali ili kufungua fursa zaidi na kuhudumia kila mahali hata maeneo yasiyo na mvuto kibiashara.

Ni haki ya kila mkazi nchini kupata huduma za mawasiliano ikiwemo huduma za msingi za posta. Tunahitaji kuzingatia Sera zinazohakikisha upatikanaji wa huduma za posta kwa wote, hasa kwa jamii zilizo mbali maeneo ya vijijini na yasiyo na mvuto kibiashara ambayo hayana huduma za kutosha. Hii inahusisha kuongeza mtandao wa posta, kuboresha miundombinu, na kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa ili

kuhakikisha kila mtu popote alipo bila kujali umbali au uwezo wake, anapata fursa ya kutuma na kupokea barua, kupata taarifa, na kushiriki katika uchumi wa kidijitali.

Tunapojitahidi kuwa Sekta jumuishi kwa maendeleo endelevu, lazima pia tuwe wasimamizi wa mazingira yetu. Sekta ya posta ina jukumu la kuwa na mikakati endelevu inayopunguza athari kwa mazingira. Hii ni pamoja na kuwekeza katika teknolojia zisizoleta madhara kwenye mazingira, kupunguza taka zisizoweza kurejelewa na matumizi ya vifungashio ambavyo ni rafiki kwa mazingira. Kwa kutilia mkazo suala hili, si tu tunalinda dunia yetu, lakini pia tunaimarisha sifa ya Sekta ya Posta kuwa ni Sekta inayojali jamii.

Ili kufikia malengo yetu, lazima tuwekeze katika nguvu kazi tuliyonayo. Programu za kujenga uwezo na mafunzo ni muhimu ili kuwajengea wafanyakazi wetu ujuzi unaohitajika kukabiliana na mabadiliko katika Sekta ya Posta. Kwa kukuza utamaduni wa kujifunza mara kwa mara, tunaweza kuhakikisha kwamba wafanyakazi wetu wapo tayari kukabiliana na fursa mbalimbali na mahitaji yanayobadilika katika kutoa huduma bora kwa wateja.

Hakuna taasisi inayoweza kufikia maendeleo endelevu peke yake. Lazima tuhamasishe ushirikiano kati ya Serikali, wadau wa Sekta Binafsi, Taasisi za Kiraia, na Mashirika ya Kikanda na Kimataifa. Kwa kufanya kazi pamoja, tunaweza kubadilishana uzoefu, kuunganisha rasilimali, na kuwa na mikakati ya pamoja katika kushughulikia changamoto zinazokabili jamii zetu.

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa sasa inakamilisha mapitio ya Sera ya Taifa ya Posta ya mwaka 2003. Sera inayorekebishwa inakusudia kukuza uwekezaji, kurahisisha biashara, na kuunganisha wadau wote katika Sekta ya Posta. Madhumuni makuu ya Sera hii ni kutumia mfumo wa posta kwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi na kusaidia mawasiliano ya kidijitali na usafirishaji wa barua, vifurushi, vipeto na mizigo miongoni mwa Sekta zote. Aidha, itakuwa chachu ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi na kuchangia katika kutimiza malengo ya Taifa.

Kwa kumalizia, naomba nirudie kusisitiza na kutambua mchango wa Umoja wa Posta Afrika (PAPU), Taasisi ambayo Tanzania inajivunia kuwa mwenyeji, tumejizatiti kuunga mkono shughuli zinazofanywa na Umoja huu kwa manufaa na ustawi wa kijamii na kiuchumi na kuunganisha bara la Afrika.

***Ninawatakia maadhimisho mema ya Siku ya Posta Afrika yenye mafanikio na ninatarajia maendeleo endelevu kwa Sekta ya Posta ya Afrika***